



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



Dar es Salaam, 19 Septemba, 2022

TAARIFA KWA UMMA

KUFUNGULIWA KWA AWAMU YA TATU YA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA KWA MWAKA WA MASOMO 2022/2023

1.0 UTANGULIZI

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma na wadau wa Elimu ya Juu nchini kuwa Awamu ya Pili ya Udahili kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini kwa mwaka wa masomo 2022/2023 imekamilika. Majina ya waombaji waliodahiliwa katika Awamu ya pili yanatangazwa na vyuo husika.

2.0 WAOMBAJI WALIODAHILIWA KATIKA CHUO ZAIDI YA KIMOJA

Waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja katika Awamu ya Kwanza na ya Pili wanahimizwa ***kuthibitisha udahili wao katika chuo kimojawapo kuanzia tarehe 19 hadi 25 Septemba, 2022*** kwa kutumia namba maalum ya siri iliyotumwa kwa ujumbe mfupi kupitia namba zao za simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili. Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo, wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kuweza kujithibitisha katika chuo husika.

Uthibitisho wa udahili unafanyika kupitia akaunti ambayo muombaji alitumia wakati wa kuomba udahili. Orodha ya majina ya waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja imewekwa kwenye tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).

3.0 KUFUNGULIWA KWA AWAMU YA TATU YA UDAHILI 2022/2023

Tume inatangaza kuwa ***Awamu ya Tatu ya udahili wa Shahada ya Kwanza kwa mwaka wa masomo 2022/2023 imeanza leo tarehe 19 hadi 25 Septemba, 2022.*** Tume inasisitiza kuwa waombaji ambao hawakuweza kutuma maombi ya udahili au hawakufanikiwa kudahiliwa katika awamu zilizopita kutokana na sababu mbalimbali, watumie fursa hii vizuri kwa kutuma kwa usahihi maombi yao ya udahili kwenye vyuo wanavyovipenda. Tume inaelekeza Taasisi zote za Elimu ya Juu nchini zinazofanya udahili wa Shahada ya Kwanza kuendelea kutangaza programu ambazo bado zina

nafasi. Aidha, waombaji na vyuo wanahimizwa kuzingatia utaratibu wa udahili kwa Awamu ya Tatu kama ilivyooneshwa kwenye kalenda ya udahili iliyo katika tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).

4.0 WITO KWA WAOMBAJI UDAHILI

Waombaji udahili wa Shahada ya Kwanza wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusu udahili au kujithibitisha katika chuo kimoja yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika. Kwa wale ambao watapata changamoto katika kujithibitisha, vyuo vyote vimeelekezwa kupokea taarifa zao na kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa.

5.0 TAHADHARI

TCU inawaasa wananchi kuepuka kupotoshwa na watu wanaojiita mawakala au washauri wanaodai wanatoa huduma ya jinsi ya kujiunga na vyuo vya Elimu ya Juu hapa nchini.

Imetolewa na:



Prof. Charles D. Kihampa

KATIBU MTENDAJI

TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA